The Speaker (Hon. Mwambire): This translates to the fact that the amendment by hon. Ngirani has not seen the light of the day. So, we are now going back to the main Motion for deliberations, honourable Members. So you can put your requests so that we can proceed with the deliberations of the main Motion. Hon. Thomas Mumba Chengo, the Leader of Minority.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Mr. Speaker, I am more than delighted to stand before this House again after having shut down a missile that had been directed at this Motion. Let me take this opportunity first to thank those who have shared that moment with us and for our colleagues, we shall have another day.

Mr. Speaker, the Motion before us here is on this Report on the Sectoral Committee on Devolution, Public Service and Disaster Management on the Internal Advert of the County Public Service Board. I had a good time with the Report, and I want first to acknowledge the Committee for taking their time to at least do this Report. Mr. Speaker, having gone through this Report, there are a few issues that I would like to bring to the attention of this House, Mr. Speaker.

I will go straight to the findings. That is on page 10, item number 5.0, which talks about the Committee’s findings. After many deliberations, having considered the oral submissions as well as the documents adduced, the Committee made the following observations and findings on internal recruitment. Number one, Mr. Speaker, the Board published an internal recruitment advert on the website and shared it on different social media platforms. That is very correct and I do not see any wrongdoing with that. The Committee did a very good job there.

Number two, Mr. Speaker, that the action of the Board in shortlisting candidates who are not affiliated with any Department of Kilifi County flawed the recruitment process.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mr. Speaker, on finding number two, going through this Report, there is an annexure there of the list of all those candidates who are shortlisted. If you look at that list, it will tell you the table is just serial numbers, the name, gender, sub-county or ward or time, Mr. Speaker.

There is nowhere to specify whether they are employees of the county, or they are not employees of the county. So, if the Committee could have gone further to annexure a document that specifies who is an employee and who is not, it could have added more weight to this finding number two, Mr. Speaker. But looking at this document as it is, Mr. Speaker, that finding is still null and void. It has no weight.

Mr. Speaker, they could have seen, or they could have gone through such kind of names, maybe but a piece of advice, Mr. Speaker, such documents must be also attached to the Reports to add more weight to any findings that they get in their due process as a Committee. In future, it will play a major role in making sure whatever is added, and the Report has more weight, Mr. Speaker.

Having said that, if we go to number three the recruitment process was discriminatory in nature, not open and transparent hence denying the public equal opportunity for employment. This is just a mere statement because there is nowhere in this Report that indicates anyone who was denied an opportunity or there is no transparency, Mr. Speaker, whereas number one tells us, first the advert was on the website and was shared on different social media platforms. If there was no transparency then the advert could not have been shared. So, the weight of this point has been nullified by their findings number one. If you go to number four, the objectives of the County Public Service Board concerning staff establishment within the County can be realized through the digitalization of either internal or external recruitment depending on which method was used, and the first one has been used therefore number four has no issue.

The four findings which are here cannot bear enough weight that is required to convince this House that the process had an issue. Mr. Speaker, going forward to the minutes attached, if you go to minute 10108DV/20/24 talking about the suspension of the internal recruitment process of the County Public Service Board, I want to applaud the level of the internet and how we embrace the internet and many other advances in social media and all the developments done by the internet. If you recall during the golden days, you could not know the gender of your kids until she or he was born. Mr. Speaker, nowadays it is easy to identify the gender of your kid because there is ultrasound and many other methods.

Mr. Speaker, in this case, I want to applaud the Committee because it also followed that route and in doing so, they went further to say the process had involved people who were not staff of the County Government. Failing to identify them and show us through the Report, to me is crucial at this stage we are not talking of employees, we are talking of Candidates who were shortlisted. Whether she or he works with the County Government at this stage does not matter most; what matters is after they have been recruited successfully. As we speak, we are talking of individuals who have appeared before a panel, have they been recruited? The answer is no.

They are still candidates. I can tell you for sure that many of us have gone through various panels and I am sure many of those panels were unsuccessful. Were they employed? The answer is No! As we speak now, the Board has not done anything wrong because they have not recruited these people. Mr. Speaker Sir, the Committee is jumping the gun. Can you wait and see if those people you purport that are not in this County Government are recruited? You cannot see me at your gate having not stolen anything and call me a thief. The Board in its nature as an independent body is doing its duty and mandate. Members, let us wait; we are doing a good

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

thing, and the Committee is doing a commendable job but at that stage, we cannot judge you in the corridors of justice if you have not committed a crime. What if from the list those who are picked are the staff of the County Government? What will we do with the Report?

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Ngirani.

Hon. Ngirani: Mr. Speaker, the Member on the Floor is saying the Board has not done anything wrong. Maybe he can tell the House the first step the Board took from recruiting externally and the advert was internal, was that not a mistake? Thank you.

The Leader Minority (Hon. Mumba): Mr. Speaker, Sir, I do not know whether it is a question and answer because we do not do questions and answers here. I want to remind hon. Ngirani that so far no one has been recruited and that is the statement.

The Speaker (Hon. Mwambire): Just go on, hon. Chengo (Mumba)

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Thank you very much, hon. Speaker, for the protection. I know very well it is an attempt to divert me from the points I am giving out. If you go down that paragraph, the only thing they have highlighted as a violation, and I have said no violation has been committed by this Board. You see they are talking of... let me read this Statement, "Some of the shortlisted candidates for interviews had not been affiliated with any Department within the County Government of Kilifi. Given that this advert had been indicated for internal candidates only, this situation could constitute a violation of Section 65(1) A. Mr. Speaker, I hold the highest book of this Country, and this is the Constitution of Kenya, 2010. If you allow me, I will refer to section 65(1) A..."

(Loud consultations)

The Speaker (Hon. Mwambire): Maybe before hon. Chengo (Mumba) reads I have ruled hon. Ngirani is out of order because there is no point in question. If he wanted to inform him he could have asked if he was willing to be informed. Members, I believe there will be no Member who will come through that route, let us stick to the laws. Proceed, hon. Chengo (Mumba).

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Thank you, Mr. Speaker. I am reminded it is the County Governments Act, 2012 but I have left it in my office. I will refer you to Article 10 which talks about Standards, Values and Principles of Governance. This Article binds organs and State Officers, Public Officers and any persons. According to the Report, I do not see any problem with that. No violation whatsoever so far has been done to that effect.

If you go to 27(4), says "...shall not discriminate directly or indirectly any person or any ground including sex, race, pregnancy, material status, health status, ethnicity, social origin, colour, age, disability, religion, belief, culture, language or birth." I believe your ears are very clear, there is no violation or whatever is conducted or done by the Board. If you go on to 56(c) and 232(1), the story is the same. I do not want to labour much but again I have a very serious concern here.

If the Committee was allowing this Report to be mutilated here before this House, as you have seen, that tells you there is something wrong. If they were clear with what they have commented on in their Report, they would not be struggling to mutilate their Report and purport to bring an amendment through the back door this afternoon, Mr. Speaker. That tells you there was a problem, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Mwambire): Let it be on record that the one who brought the amendment is not a Member of the Committee, first....

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Leader of Minority (Hon. Mumba): I said they allowed it to be mutilated. I did not say the Committee mutilated it. Get me right, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Mwambire): Just stick to that because this Report is for the Assembly. It is no longer for the Committee.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Mr. Speaker, I am guided, but the Committee allowed it here because they did not deny it...

The Speaker (Hon. Mwambire): No, the Mover did not allow it. So, please just stick to that so that you can conclude.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Mr. Speaker, as I conclude, so that you may not assist them, Mr. Speaker, I heard someone talking of the County Assembly being involved in a violation of law...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Mr. Speaker, it has been said by the Member who stood on the Floor that an amendment has been brought into the Chamber through a backdoor. I want to understand this backdoor because I know the one who has tabled the amendment has followed the Standing Orders of this House. So, let me understand clearly what this backdoor the Minority Leader is talking about.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): The language is very difficult to understand sometimes. I say thank you for the guidance that you have given. Maybe guidance to her does not mean anything. I want to finish by saying, Mr. Speaker, as you have guided, the County Assembly...

The Speaker (Hon. Mwambire): I hope hon. Mumba did not talk about the backdoor.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): You've guided, Mr. Speaker, on that.

The Speaker (Hon. Mwambire): Okay.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): As I conclude, Mr. Speaker, I overheard the County Assembly is nowhere...

(Loud consultations)

Why are you getting jitters? You will have your time. Allow me to finish.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Mumba, you are a ranking Member of the House. So, just do it well so that it can be in the record? The Speaker normally does not have ears and does not have eyes. He is guided by Members. So, if a Member feels that you have said... That is why I have asked whether it is true you have talked about a backdoor. For me, I do not have ears. I normally hear from Members if they tell me that is the position.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): It is a parliamentary language.

Hon. Members: No, no, no.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Mumba, if you have used that word, just withdraw that word; it is not good for the Assembly. Just the same way hon. Ngirani used that word which is not parliamentary.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): I respect your ruling...

The Speaker (Hon. Mwambire): The amendment which has come to this Assembly was well approved and we have concluded it. It did not see the light of the day. We do not need even to talk about it now. Let us stick strictly to the Motion before us so that we create a conducive

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

environment for the issues to flow and be well understood by Members. Hon. Member, do not even quote about the amendments here because they have not seen the light of the day.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): We have passed that, Mr. Speaker, but in court, we have things called precedencies, Mr. Speaker, and they are even used in the future to give directions and rulings in matters that come in court, Mr. Speaker. So, as you have guided, Mr. Speaker, let me conclude.

Mr. Speaker, I have heard someone saying that this Assembly does not want to be involved anywhere in violation of the law. Let me be very categorical, Mr. Speaker, here...

Hon. (Ms.) Grace: Mr. Speaker, I am the Member who...

(Loud consultations)

The Leader of Minority (Hon. Mumba): Protect me, Mr. Speaker, so that I conclude. They are just wasting more time.

The Speaker (Hon. Mwambire): I have ruled on that one unless he repeats. So, conclude, hon. Mumba. The Board is very independent. It will carry its cross once it violates any law. So, there is no way I want this to be quoted very clearly, that this Assembly will not be involved in any wrongdoing by the Board.

The Leader of Minority (Hon. Mumba): I want to just set the record straight that the Assembly has its role, and the Board has its role. Whenever the Board goes astray, it will have to carry its cross. With the many remarks, Mr. Speaker, I want to say, let this Motion on this Report suffer the same fate as the amendments are made. I strongly say, go to hell with this Report.

PROCEDURAL MOTION

EXTENSION OF TIME

Hon. (Ms.) Koki: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I stand to move a procedural Motion on the extension of time until the conclusion of Business.

THAT, pursuant to the provisions of Standing Order 27, (3A), read together with 50(M), this House resolves to extend the sitting time until the conclusion of Business appearing on the Order Paper.

Thank you, Mr. Speaker. I call upon hon. Twaher to second.

Hon. Twaher: I second, Mr. Speaker, Sir.

(Question proposed)

(Question put and agreed to)

Hon. (Ms.) Sidi: I stand to support the Committee. Mr. Speaker, when you go through this Report...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Twaher.

Hon. Twaher: Is it supporting the Committee or the Motion, Mr. Speaker?

Hon. (Ms.) Sidi: The Motion, sorry. Now, on page nine of this Report, page nine, 4.0, paragraph two on submission by the County Public Service Board. This is what the County

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Service Board Chair submitted when he came to the Assembly. He said that the Committee was informed that the County Public Service Board has identified departmental staffing needs due to retirement, death, and long-term contractual employees to ensure effective and efficient service delivery.

It was deemed necessary to conduct internal, and the word here is 'internal' recruitment. This approach was aimed at appreciating staff that had the necessary qualifications and also addressing the issue of an inflated wage bill. The Board is currently working on streamlining the employment and staff placement process which plans to ensure external advertising soon.

First, I wanted to go on record that both the people; the casuals and the ones who are not the casuals, are all from Kilifi. That is one thing we should understand, and also people should understand that the fact that your person is on this list does not mean they have gotten employment.

It is still a list waiting for interviews. Mr. Speaker, these casuals have been in this county for a very long time. They have suffered without payment and are still working with us. Most of them are in our hospitals. What I wanted to urge the House is all these people are our people. The casuals and those applying are also ours. Let us give priority to the casuals because they are already in the system. We might want to employ other people but we have to start training these people first.

We need money for training; in fact, the wage bill for casuals will not be high because they are already in the system. We will just need a few allowances that will be increased. But that notwithstanding, if we bring in a new person; we need to pay this person. Have we put a budget for this new person to come in? I want to urge Members; I know you are here probably there is pressure from...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Hassan.

Hon. Hassan: Asante, mheshimiwa Spika. Labda ningeuliza, maanake naona nashangaa, kuna mfanyikazi yoyote wa kibarua aliyekatazwa ku *apply* nafasi ambayo ataandikwa kazi? Kwa sababu, sijaona. Asante.

Hon. (Ms.) Sidi: As we have said, Mr. Speaker, we do not answer questions in this Assembly...

The Speaker (Hon. Mwambire): I said just proceed, maybe the one who is going to respond will take care of such issues, proceed.

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you. My take is this; kindly let us absorb the casuals first then... because I also want to believe there are casuals from Kayafungo Ward who also want to be absorbed. There are people from Kayafungo Ward who have also applied. All of them are our people. So, kindly let us think about our people and not our selfish interests. Thank you, Mr. Speaker.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Hoja hii. Nasimama kupinga Hoja hii iliyoletwa na Kamati ya *Devolution*. Nimeongea kuanzia mwanzo ya kwamba jambo la wafanyikazi tusiliweke siasa, jambo la wafanyikazi tusiliweke mzaha, jambo la wafanyikazi lazima tulichukulie kwa hekima. Nimekuwa katika Bunge hili wakati Ugatuzi ulikuwa unaanza; Bunge la kwanza na hili ni Bunge la tatu. Wewe ukiwa ni Naibu wa Spika na tukisaidiana na wewe, Bw. Spika, tunajua changamoto zile ambazo zinapata wafanyikazi katika jimbo letu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Bw. Spika, nataka kusema ya kwamba Kamati haikufanya vibaya kuita *County Public Service Board*; walifanya vizuri sana na mimi kama Kiongozi wa Wengi Bungeni, nataka kuwapongeza na niwashukuru. Lakini baadaye Kamati kusema ya kwamba wameamua majina ambayo yametolewa yafutuliwe mbali, hapo ndio Kamati ilikosea, Bw. Spika. Ndio nimetangulia kusema ya kwamba swala hili sisi kama wanasisia na nina amini ya kwamba hapa leo hii Bw. Spika, kuna wafanyaji kazi, vibarua, wametoka tabaka mbali mbali hata wengine wanaweza kukubaliana na mimi hata nauli wameomba ili kuja kusikia mipangilio ambayo inazungumziwa hapa.

Leo hii, sisi waheshimiwa hapa hakuna mheshimiwa amekosa kiamsha kinywa, chakula cha mchana na wala chakula cha jioni lakini wako wafanyikazi wa Kaunti ya Kilifi wamekosa chakula, Bw. Spika, ndio ninasema swala hili linataka umakinifu. Swala hili linataka mipangilio. Bodi ya kuajiri wafanyikazi ikiongozwa na Bw. Mturi tuliwa *vet* sisi na wakati tuliwapitisha na Bodi iliyokuwepo ilipitia hapa na sisi tukaiangusha Bodi ile ndio tukachagua Bodi mpya.

Bodi ambayo tunaizungumzia saa hii, iko kwenye kazi karibia miezi kumi hawajapitisha hata mwaka mmoja tangu wachaguliwe. Angalia kwa muda huu mchache Bodi imekaa ikaona ya kwamba wafanyikazi katika jimbo letu la Kaunti ya Kilifi wako na shida, wanapata shida na hawaandikwi. Wamekaa wakafuata sheria. Sheria ya kwanza ni kutangaza zile kazi. Sheria ya pili ni kufanyiwa *interviews* wale walioorodheshwa. Waliongea ya kwamba kwanza watawapatia kipau mbele wale ambao wanafanya kazi katika jimbo letu.

Bw. Spika, kwa kusema hivyo ni kwamba kuna wafanyikazi katika Jimbo hili wamekuwa vibarua zaidi ya miaka kumi. Kuna watu wamejitolea kufanya kazi bila ya malipo. Kwa hivyo, Bodi ikawapa kipaumbele hawa ndio kwanza wachukuliwe na watu wa kutuma maombi ya kazi. Wale waliotuma maombi, waliorodheshwa. Hakuna mheshimiwa ambaye amekuwa amehusika na hilo. Mtu akiwa kwenye orodha, si kwamba amejiriwa kazi; orodha iliyotolewa kupitia Katibu wa Kamati nilipoiangalia nikasema tusidanganye wananchi. Hapa aliyeleta *amendment* mheshimiwa Ngirani na amesikika na kila mtu amesema yeye mwenyewe aliambia wananchi wake wasi *apply* hizi kazi. Lakini leo hii ukiangalia hii orodha kama kuna mtu amenufaika ni mheshimiwa Ngirani. Mheshimiwa, nimehesabu namba ya watu wako katika wadi yako wameorodheshwa ni watu thelethini na tisa (39). Kuna waheshimiwa ndani ya Bunge hili hawana mtu hata mmoja...

The Speaker (Hon. Mwambire): There are some interventions from Hon. Ngirani and hon. (Ms.) Sidi.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Mr. Speaker, do they want to inform me or?

The Speaker (Hon. Mwambire): We want to hear from them. Just take a seat. Let us hear in case they will want to inform you, I will ask you so that you know. Hon. Ngirani, kindly proceed.

Hon. Ngirani: Mr. Speaker, the hon. Member is saying that in the shortlisting...

The Speaker (Hon. Mwambire): Are you informing him or? We want to understand.

Hon. Ngirani: I am not informing him. I am trying to protect myself from allegations that ...

The Speaker (Hon. Mwambire): You will get an opportunity. Do not worry. Just take your seat.

Hon. (Ms.) Sidi: *Thank you. Majority Leader, amesema hiyo list haimaniishi kwamba watu wameandikwa kazi. Halafu yeye bado anasema watu 30 wanatoka Ganze, sasa sielewi hapo.*

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Ndio nikasema hapa kuna watu na waheshimiwa. Ninayosema ndio haya, mheshimiwa Spika.

Hon. (Ms.) Sidi: Maybe a clarification...

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Ibrahim, everyone in this Chamber is an hon. Member.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Not all of them ...

Hon. (Ms.) Sidi: It starts with you *mheshimiwa*.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): I can tell you who will not be a member in 2027.

(Loud consultations)

The Speaker (Hon. Mwambire): Okay, proceed so that we avoid these sideshows.

Hon. Rafiki: Thank you, hon. Speaker. As much as I respect our Leader of Majority, I think it is more mature for him to apologize to this House because you are here as hon. Members all of us equally. The word of saying *kuna watu na waheshimiwa* is not a respectful language to this House. I respect him, and I love him but kindly, Mr. Speaker, allow me to request him to apologize to this House. Thank you.

The Speaker (Hon. Mwambire): Please withdraw a little, Majority, so that we can make the environment okay. I know you are not that close to God to even know about 2027, so just withdraw that word so that every Member can be comfortable.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Bw. Spika, ukinipa muda ili nifafanue vizuri kwa sababu kuna mambo ...

The Speaker (Hon. Mwambire): Just withdraw. Withdraw and apologize, and you proceed so that we save time. I know some issues require a lot of time. I know how sometimes you can make people laugh and how you can make the Assembly also feel warm.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): So what should I withdraw? Just tell me.

The Speaker (Hon. Mwambire): The Member claims that you said there are some hon. Members and there are people in the House.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): That is very correct, Mr. Speaker. *Kuna watu hapa juu mheshimiwa...*

The Speaker (Hon. Mwambire): We are talking about the Chamber.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): No, no, no, I did not say anything about the Chamber, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Mwambire): Just withdraw.

(Loud consultations)

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Mr. Speaker, I did not say, Mr. Speaker, do I look mad to say that there are people here who are honourable? Nimesema kuna watu na waheshimiwa and that is very correct, sasa hawa si watu?

The Speaker (Hon. Mwambire): We do not address people in the gallery. We address the Chamber. So just withdraw.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Okay, I withdraw.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Laughter)

The Speaker (Hon. Mwambire): Okay, Proceed.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Bw. Spika, tunakushukuru vile unapeleka Bunge hii na tunakupongeza sana. Nataka kusema kwamba nimepata pia changamoto kwa Bunge hili na mimi nashukuru wale wenzangu ambao wamesema ya kwamba kuna watu ambao waliandikwa hapa ambao hawakuwa *internal* na *external*. Sasa mimi kama *Majority Leader* nataka kuhakikishia Bunge hili kwamba hili ni jambo ambalo mimi na uongozi wa Bunge hili tutaendelea kulifanyia kazi kwa sababu nimeona, lakini watu hao si wakawa ni watu wale wa Ngirani.

Bw. Spika, nataka kusema hivi na ninataka kutoa maombi ambayo pia, Bw. Spika, ninakuomba pia wewe kama kiongozi na Spika wetu, katika zoezi hili ambalo linaendelea, ni zoezi ambalo linafurahisha kila mtu ndani ya Jimbo letu. Kamati husika ninaomba tuko na waheshimiwa ambao ni wachapakazi ndani ya Bunge hili na siku mswada kama huo pia ukiletwa mimi ninaona utaungwa mkono mia kwa mia.

Hii Kamati ningewapatia ushauri wa kwamba *instead* ya hawa kusema hii *programme* isiendele, wapange mipangilio mwafaka kwanza tujue wale ambao ni vibarua katika jimbo letu la Kilifi ni wangapi.

Pili, Bw. Spika, tutawezaje kuwasaidia wale vibarua waandikwe kazi wawe *permanent*? Hilo sio suluhisho zuri. Wakati tukifikia mahali kama hapa, hakuna haja ya chuki, mambo ya wananchi wa Kilifi kuandikwa kazi tusileteane mzaha na chuki kwa sababu haya ni manufaa ya familia na ni manufaa ya jimbo letu; ni manufaa ya kila mtu kwa sababu si haki leo mtu akae zaidi ya miaka kumi ni kibarua leo *County Public Service Board* imejitolea kufanya kazi sisi tunasema kuanza kusimamisha.

Unajua *process* ya serikali kutoa tena *advert* ya watu kuandikwa kazi tena, leo tukisema hao wasiandikwe utafikiri si mambo ya kesho, ya kesho kutwa, ya wiki ijayo, ya miezi ijayo, ni mambo ya mwaka ujao. Kulingana na kwamba hatuwezi kuwasukuma kuwaambia mbona hamuandiki au mbona hamu-*advertise*? Kwa hivyo, mimi nataka kusema kwamba wale ambao maanake leo, Bw. Spika, nimepambana na waheshimiwa katika ofisi yangu na wengine tumeangalia hii *list* na mheshimiwa mmoja anaangalia anasema hawa siwajui. Si maswala ya kujua mtu hapa. Hapa ni maswala ya huyu ni wa Kilifi ama si wa Kilifi? Je, huyu amekuwa akifanya kazi kwa Kilifi Kaunti amedhulumiwa ama hajadhulumiwa? Hayo ndio maswala ambayo tunatakikana tuyaongee.

Bw. Spika, mimi nikimalizia ninasema ya kwamba wananchi wa Jimbo letu wanatuangalia. Haki zao ziko mikononi mwetu. Haki zao ziko kwenye Bunge hili. Tuwacheni ugomvi na tushirikiane kwa manufaa ya wananchi wetu. Kama mimi *Majority Leader* umeona nimefanya makosa ni vizuri unakuja unani-*advise*. Sisi binadamu si kamili na kila mtu anafanya makosa lakini kitu kizuri ni ule ushirikiano na uelewano. Hakuna siku mwananchi wa Kilifi hatapata faida kama kutakuwa na mgawanyiko katika Bunge hili. Hakuna siku mwananchi wa Kilifi ataandikwa *permanent* kama kutakuwa na mgawanyiko katika Bunge hili. Na mambo, Bw. Spika, nataka uwaeleze pia waheshimiwa, kupiga *yes* na *no* huwa ni kawaida katika Bunge. Katika Bunge ni lazima kuwe na msisimuko kwa hivyo hata mtu akipiga *yes* tusiwekeane chuki.

Kwa hivyo, mimi nataka kumaliza hapo. Nitaifanyia kazi Ripoti hii bora tu la zaidi tusirudi hapa tukalumbana tena ama tukalaumiana. Asanteni. Kwa hayo machache, Mungu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

abariki Bunge hili, Mungu abariki Spika wetu na wale ambao mimi nimepinga tena vikali sana hii Ripoti, naunga mkono *process* iendelee ili watu wapate kazi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Asante, mheshimiwa Spika. Nataka nianze kwa kusema kwamba kule nje kuna kilio na kilio ni cha haki; haki ya wafanyakazi walio katika ajira ya vibarua katika gatuji hili. Wenye kushikilia haki hii ni sisi tuliomo ndani ya Bunge hili na wale watendaji ambao tunawaitia *Executive* ndio wameishikilia haki ya hao vibarua ambao wanalia kule nje. Nataka niendelee kwa kusema, Tume ya Waajiri hapa kwetu nchini imesisitiza sana kwamba, magatuji yote ndani ya hii Kenya yaweze kuachana na kuajiri vibarua.

Wale watu wote waweze kuajiri kwa mfumo wa *permanent and pensionable* ambao tunaita Kiswahili ni ajira ya kudumu kisha yenye pensheni. Huo ni muongozo kutoka kwa tume ya waajiri hapa nchini kwetu. Swali ni orodha ya majina haya ambayo leo tunayajadili hapa Bunge yameletwa kwa kufuata taratibu zote ambazo Bodi ya wajiri katika Gatuji letu la Kilifi iliweka katika tangazo hili? Jawabu ni la kwa sababu tangazo lilikuwa linazungumzia kuhusu *internal* waajiri wale watu ambao wako pale ndani.

The Speaker (Hon. Mwambire): We have an intervention from hon. Ibrahim.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika...

Hon. (Ms.) Mapenzi: Under which Point of Order?

The Speaker (Hon. Mwambire): Just hold on. We want to hear from him.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika. Kama vile nilivyoenena na nina mnukuu mnenaji aliyenena. Unajua mheshimiwa Elina Mapenzi alikuwa ni mwalimu na walimu huwa wako na ufahamu mwingi sana. Nimemsikia akisema kwamba tume ya uajiri walitoa muongozo. Sijui aweza nielezea ili na sisi tufahamu tuwe tuko nao sijui walitoa huo muongozo lini na walitumia kipengele gani ili na sisi tujue? Tupate faida maanake ameongea neno la maana sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Tete, you have an intervention. Is it Tete or Twaher?

Hon. Twaher: Samahani, Bw. Spika. Mheshimiwa Elina anasema *County Public Service Board* imevunja sheria. Naomba kuelezewa ni sheria gani imevunjwa hapa?

Hon. (Ms.) Mapenzi: Umesema tusijibu watu hapa Bungeni. Mimi nitaendelea. Sasa mheshimiwa Spika, nitaendelea tume ya Uajiri ya Gatuji la Kilifi imeenda kinyume na tangazo waliloliweka la uajiri wa hawa watu. Maanake kama tangazo liliwekwa kwamba wale waliwekwa ndani waweze kutafuta hizi nafasi nikiangalia hii orodha hapa kuna Kibore Jerono Jecinta. Huyu ametoka Elgeyo Marakwet; *page 1, number 13* Idd Mongo Mangale ametoka Kinango Mwakubo Ward, kuna Ruth Sada Mugandi ametoka Kinango Kasemeni. Hapa kuna Mwanajuma Mohamed Hemedi ametoka Mombasa Jomvu, kuna Rosemary Mthoni Muriuki ametoka Kianjuri hao ni wachache tu nitakomea hapo...

The Speaker (Hon. Mwambire): Are they working with the county as per the advertisement?

Hon. (Ms.) Mapenzi: Hii ni tayari kwamba wametoka huko nje na hili tangazo ilikuwa ni ndani kwa ndani. Maanake si inasema hapa...

The Speaker (Hon. Mwambire): Ndani kwa Ndani haimanishi ndani ya Kilifi peke yake. Bora awe anafanya kazi ndani ya Gatuji la Kilifi.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Hawa hawafanyi kulingani na... hawafanyi. Sasa mheshimiwa Spika, tayari tukizingatia hii orodha vile ilivyo na tukienda na ile orodha vile ilivyo kuna uwezekano wale watu wetu ambao tulidhamiria kulingana na tangazo waajiriwe wana

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

uwezekano wa kukosa hizi nafasi. Wana uwezo wa kuzikosa hizi nafasi na tukizingatia kipengele cha tangazo, orodha hii inastahili kufutwa yaani ikataliwe. Kwa hivyo, mimi ninasema hivi kulingana na kazi nzuri waliyoifanya Kamati ya Ugatuzi na mapendekezo ambayo waliyapeana hapa mapendekezo hayo nafikiri kila mmoja anayaona hapa. Kama uko na ile Ripoti nitasoma kwa faida ya wana Kilifi waelewe tunafanya nini hapa, maana sisi ni watetezi wao na kama tutasimama katika nafasi ya kuwafinyilia itakuwa si haki mbele zao na hata mbele za Mwenyezi Mungu.

Kwamba, *“The recruitment process vide an internal advertisement issued on 28th March 2024 be null and void and done afresh. The County Public Service Board should facilitate the House with a Report of the staff indent.”* That is in brackets, *“(Outpost of all county departments within the six days.”*

Hii *recommendation* hatuwezi kuipinga na kuipinga ni kama tunawakatalia haki zao wana Kilifi na nataka ibainike mbele ya kila mmoja ndani ya Jimbo la Kilifi. Yule atakayesema kinyume na Ripoti hii amekataa haki za wale wafanyikazi.

Mheshimiwa Spika, mimi sitasimama katika udhalimu hata siku moja na ndio sababu sitaki kudhulumiwa; wakati wote nitasimama na haki. Maana ndio kazi iliyonileta kutetea yule mwananchi ambaye hana mamlaka. Tutumie mamlaka yetu vyema ili siku ukilala uwe na hesabu njema kule mbinguni.

Tusichukue nafasi kudhulumu wananchi. Hapa wana Kamati walikaa wenye akili zao, ziko timamu kabisa wakiongozwa na Mwenyekiti mheshimiwa Zia Kahindi aliweka sahihi kwamba waliyojadili na ndio waliyopendekeza. Mheshimiwa Lilian Vijenderwa ambaye ni Naibu Mwenyekiti vile vile akaweka sahihi kwamba hii Ripoti iko sawa na wamekubaliana na wanasimama na mapendekezo. Mheshimiwa Mariam Mkumbi, Mheshimiwa Justin Rafiki Kaingu, Mheshimiwa Naftali Nyae Kombo, Mheshimiwa Said Juma Iddi, Mheshimiwa Theophilus Kalama na Faith Jane Kea wote waliweka sahihi. Nimeenda kwa HANSARD nikauliza ni kwa nini Mheshimiwa Martha Koki hakutia sahihi, Mheshimiwa Edward Kaingu Ziro hakutia sahihi na Mheshimiwa Rashid Odhiambo nikaambiwa hawakuwepo.

Kumaanisha hawa wote walikubali na wakajadiliana kumaanisha Ripoti hii iko sahihi na walikuwa wamezingatia vigezo vyote. Mheshimiwa Spika, tusimame kutetea wananchi na kwa sababu ya kuwatetea wananchi naunga mkono Ripoti hii kwamba mapendekezo ya wana Kamati yatekelezwe na kutekelezwa kwake kutatuondolea hawa wakina Kinango, kina Elgeyo Marakwet ili Kadzo na Kahindi aliyefanya kazi miaka kumi katika mateso... maanake mara nyingine tunasikia vilio vya miezi sita bila mishahara. Halafu swali tujiulize kama leo tutaruhusu karatasi hii wale watu waliosajiliwa wakaandikwa kazi halafu kuna muda kwamba...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Koki.

Hon. (Ms.) Koki: Asante, mheshimiwa Spika. Nikinukuu aliye kwenye Sakafu akisema kuwa tuunge mkono Ripoti iliyoandikwa na Kamati na ndio tutaondoa kina Elgeyo Marakwet na sijui wapi tuko na asilimia thalathini (30%) ya wafanyikazi ambao wanatakikana kutoka sehemu nyengine, tuwache mambo ya ukabila.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Na ndio maana tulikuchagua MCA (*Member of County Assembly*) hapa Bungeni na unatoka katika jamii ya Wakamba walio wachache, kwa hivyo hatuna ukabila. Ndio maana tukakupua kura zetu...

The Speaker (Hon. Mwambire): Mheshimiwa Elina, malizia tafadhali.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Haya sasa mheshimiwa...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Koki.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Koki: Mr. Speaker, she will need to withdraw because she did not give me her vote. No, yeye si mpigaji kura wa Mariakani.

(Loud consultations)

The Speaker (Hon. Mwambire): Just hold. I beg to give an opportunity to speak but let the other Members remain silent so that you can prosecute your issue, hon. Koki.

Hon. (Ms.) Koki: Asante, Bw. Spika. Mimi nilichaguliwa na nikaletwa hapa na wapigaji kura wa Mariakani ikiwapo mheshimiwa Mapenzi ambaye simpigaji kura wa Mariakani na kama alinipigia anionyeshe kura yake na nitashukuru kama alinileta hapa Bunge.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Koki, take your position. Hon. Mapenzi, proceed.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Mheshimiwa Spika, hilo si swala la kuzungumzia na kujadili lakini kwa sababu linamsumbua mwenzangu wacha nilifafanue na uwezekano wa ku *withdraw* niko nao maana mimi ni mtu wa kushuka mimi sina shida.

(Loud consultations)

Mimi sikukupigia kura Mariakani lakini kuna mamangu, baba yangu na dada yangu walikupigia kura. Kwa hivyo, ukisema sisi...

(Hon. Koki stood in her place)

...kaa kaa, sisi wagiriama tulikupigia kura.

The Speaker (Hon. Mwambire): Just sit, hon. Koki, you are not on record. Hon. Elina Mapenzi, I think it will be in Order for you to withdraw so that you can continue.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Eeh, haya natoa kwamba nilipiga kura Mariakani Koki akaja hapa, nilipiga kura Jilore *Primary* nikampigia kura Hamisi Jambo. Asante.

(Loud consultations)

The Speaker (Hon. Mwambire): Just hold, hon. Members. You know the rules of the game. Why do you make noise? You know very well it is just a matter of putting your intervention and proceeding. Hon. Twaher, let me ask you something, just for clarity purposes. I do not think it is in order to be the Chairman of interventions because you are always on interventions. Why don't you give an opportunity to your colleagues? You are always on interventions. You have not removed it. Why intervene at that point?

(Hon. Twaher spoke off record)

You are out of Order; I have not given you an opportunity to speak just sit. Proceed, so that you can conclude.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Wanajaribu kutatiza mteremko wa hoja zangu. Sasa mheshimiwa Spika, nataka tujiulize...

(Loud consultations)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

...namalizia, mheshimiwa Spika, tafadhali.

The Speaker (Hon. Mwambire): Conclude, please.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Namalizia sasa, maanake tumeomba muda hapa tukasema ilikuwa ni ya nini. Kama sasa tutakataa Ripoti hii ya Kamati ya Ugatuzi ambao wanasimama na hii Ripoti ya *internal* wakisema itupiliwe mbali *list* hii maana haikuzingatia tangazo lili. Leo, tuikatae tuende vile mnataka. Mfano, wale vibarua ambao wako pale kaunti wakose hizi ajira halafu baadaye wapewe *contract* za mwaka ambapo baada ya hapo itakuwa *contract* imeisha.

Waheshimiwa wenzangu, tutawapeleka wapi hawa vibarua maanake tayari waajiriwa watakuwa tayari ndani wakifanya hizo kazi? Kumaanisha watakuwa hawana nafasi kufanya kazi kwa hili Jimbo letu la Kilifi, tutakuwa tunawafanyia haki? Wenzangu mbali na kuzingatia chama chako ambacho kimekuleta hapa na mbali na kuzingatia uko serikalini, simama na haki hivi leo.

Mheshimiwa Spika, vibarua hawa wame *serve* hii Kaunti kwa mateso bila kupewa ajira ndani ya miezi sita na zaidi hivi leo ni *opportunity* wakaajiriwe tunasema hatutaki waheshimiwa.

(*Loud consultations*)

The Speaker (Hon. Mwambire): Consult on low tones so that we can hear what she is saying.

Hon. (Ms.) Mapenzi: Nataka ijulikane Kilifi nzima kuwa mimi Elina Mapenzi Samini niliyeletwa hapa Bunge la Gatuzi ya Kilifi nasimama na hawa wachache ambao hawana watetezi katika Bunge hili kwamba karatasi hii itupiliwe mbali na zoezi hili lianze upya kwa kuzingatia hiyo *Memo* yao ya *Internal advert*. Thank you very much.

(*Applause*)

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, I beg to give guidelines on how we are going to prosecute this issue. We have a number of Members who have sent requests and it will be prudent for every Member to speak. I know we have extended time for everybody to speak so instead of saying the same thing using different words let us be precious and use three minutes maximum to conclude. Hon. Mkumbi (Mariam).

Hon. (Ms.) Mariam: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipa hii nafasi. Mimi kama mmoja wa wana Kamati ambayo imekuja na hii Ripoti, nasimama kuunga mkono kwa dhati Ripoti hii. Bw. Spika, niko na sababu kwa nini naunga mkono. Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na mimi nataka niende kwa *submission by the County Service Board*. Hao wenyewe waajiri na hapo nataka niwasomee kitu. Nataka niwasomea kitu kwa sababu sisi kama wana Kamati tuliuliza maswali. Iko *page nine* katika ile *submission* ya *County Public Service Board* hao wenyewe wakati tulipokuwa tumewauliza hayo maswali twende tusome hapa. "*This approach was to end at appreciating staff who had the necessary qualifications and also addressing the issue of an inflated wage bill. The Board was currently working on streamlining employment and staff placement process and external advert soon.*"

Mheshimiwa Spika, inadhihirisha kuwa hawa wenyewe walikuwa wameona kuna haja ya kufanya *External Advert* baada ya kufanya *internal*. Sisi kama Kamati tuliona makosa ni kuwa walifanya *internal advert* na walifanya kulingana na vile walieleza alivyoeleza kuwa walikuwa wanataka ku *absorb* wale *staff* ambao tayari wako kazini na hawajachukuliwa *permanent*. Walikuwa na nia nzuri ndiyo maana waka *advertise Internal*. Sisi kama Kamati tulisema iwe

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

cancelled kwa sababu ikiwa wao wenyewe walisema ni *Internal* na huwezi sema ni *Internal advert* halafu uchukue watu wa nje tayari hapo utakuwa umevunja sheria.

The Speaker (Hon. Mwambire): Observe time, mheshimiwa.

Hon. (Ms.) Mariam: Ndiyo nina *observe*. Hicho ndicho kipengele peke yake ambacho kilifanya tukaja na hizi *recommendations* badala ya kuwahoji na hao wenyewe wakakubali kuwa watafanya *internal adverts* baadaye. Unajua ukifanya *internal advert* halafu uchukue watu wa nje, halafu kuna watu wanaelewa sheria na waliona hiyo *advert* na wako na *qualifications* lakini ilikuwa imewafunga tayari hiyo ni *discrimination*. Na ukichukua watu wa nje tayari hukuwa muwazi, *Article 10 issue* ya *values and principles* mambo ya uwazi ama *intergrity* tayari umeivunja. Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tuliangalia hiyo *point* tukizingatia kuwa tunaongozwa na sheria katika Bunge hili. Asante, Bw. Spika.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Hassan.

Hon. Hassan: Asante sana, mheshimiwa. Kwanza, nataka kuchukua hii fursa kushukuru Bodi husika kwa kutupatia vibarua. Pili, kumshukuru mheshimiwa mustahiki Gavana wetu maana anajua kuna kilio cha ajira. Bado nashangaa na kujiuliza maswali mengi sana; hiki ni kipindi changu cha tatu nafikiri mkongwe zaidi ya wote hawa. Uwazi wa ajira katika vipindi vyote vilivyotangulia sikuwahi kuuona lakini kwa sasa nashukuru uwazi unaonekana. Tulikuwa tunaona watu tu wameajiriwa. Leo tumepewa nafasi ya ajira, wale walio ni wa nje ni kama watu wawili waliotajwa. Naomba tu kwa unyenyekevu hii *procedure* iendelee. Nimesimama kuipinga Hoja hii. Naomba Bodi iendelee na kazi yake.

Hon. (Ms.) Grace: Asante, Bw. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Nitafwata sheria yako ambayo umesema tuchukue muda mrefu na kwa sababu mimi ndio *Minority Whip* nafaa kuwa mfano katika Bunge hili. Nasimama kuunga mkono hii Ripoti ya Kamati asilimia mia kwa mia na baada ya kuipitia nilitaka kujua zaidi ni nini ambacho ninafanya hii Kamati ipinge *the shortlisting of the candidates*.

Nilipata hiyo *list* na tangazo lililowekwa ni *internal advert*. Kwa kuelewa kwangu ina maanisha wafanyikazi ambao tayari wanafanya kazi na Kaunti yetu. Matarajio yangu ilikuwa ni wale walioko *whether* ni *casuals* ama *permanent at least* wawe *shortlisted* katika ile *list* lakini cha kushangaza, mheshimiwa Spika, na nitatoa mfano, kuna mheshimiwa mmoja amesema kuwa anashangaa watu wawili pekee ndio waliotajwa kuwa sio wafanyikazi wa Kaunti kufikia sasa, lakini kulingana na *list* naona ni zaidi ya watu Hamsini (50) ambao hawako katika kaunti. Nasikitika sana, mheshimiwa Spika...

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Radhia.

Hon. (Ms.) Radhia: Hawa watu wa nje ni wa aina gani?

The Speaker (Hon. Mwambire): Unataka kufahamishwa ama kumfahamisha?

Hon. (Ms.) Radhia: Nataka kufahamishwa mimi.

Hon. (Ms.) Grace: Ndio naendelea kuelezea, Bw. Spika. Mheshimiwa Radhia, ungenipa muda kwanza. Nikisema watu wa nje namaanisha, anaweza kuwa ni mtu wa Kilifi lakini hafanyi katika *County Government*. *Internal advert* ina maanisha huyu mtu awe ni Kazungu awe ni Karanja au Adhiambo lakini anafaa kuwa anafanya kazi katika Kaunti.

Inasikitisha, nitatoa mfano mmoja wa Anthony Thaura Bao, huyu ni mwana Kilifi kutoka Chasimba, mwingine ni Thregatsh Munga Mwarome, huyu ni mwana Kilifi kutoka Chasimba lakini anafanya Rea Vipingo plantation. Hiyo *plantation* haiko katika Idara ya Kilifi Kaunti. Naunga mia kwa mia hii Ripoti.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Loud consultations)

Rea Vipingo iko Katika Kaunti ya Kilifi lakini *it is a private company not County Government workers.*

The Speaker (Hon. Mwambire): Hii Ripoti ambayo unasoma iko katika ile Ripoti ambayo tunajadili leo ama?

Hon. (Ms.) Grace: Ndio hiyo hiyo. Bw. Spika, nasikitika sana mimi nimetoka Gede na kuna Gede Sub-County Hospital na hapa kuna mtu anaitwa Fatuma Gatiwani Mohammed from Tana Delta wachu Otha, Otha Dispensary Tana River County; huyu sio mfanyikazi wa Kaunti, pale Gede Dispensary kuna Kadzo na Katana hajapata kazi na hajakuwa *shortlisted*.

Hon. Kubo: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for this opportunity. I stand to oppose this Motion. I have four reasons for opposing it. Number one, the Committee did not do complete work; they could have separated the internal and external shortlisted candidates.

Two, they have indicated in their findings that the interview was discriminatory, but I do not understand this because I have gone through the shortlisted candidates, and I have seen the people from my ward.

Number Three, we have run short of time. Our casuals are suffering, and we need to do something to make sure they are employed. Lastly, the Chairperson and the Vice-chairperson both ran away; they are not here.

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Kubo, in my Office, the Report I have is that the Chairperson is hospitalized. He has been in hospital for over one and half weeks now. So, please it is unfair to say that because today it is him who is unwell tomorrow...

(Loud consultations)

Hon. Members, I do not have any authority to ban any Member from either coming or leaving. There are Members who are here now but will not be here next week. Should I stop the discussion to inquire where they are? I think what we do, we will ring the Bell in case a member comes, and that will be okay. If a Member does not come, we will proceed so long as the Members have a quorum.

Honourable Members, I am trying as much as we can to save time. We will ring the Bell when it comes to voting.

Hon. Ngirani: Mr. Speaker. I stand in support of this Report with the following statement: Number one, using the findings of the Committee. The Board published an internal recruitment advert on the website and shared it on different social media platforms.

That is internal recruitment. Again, the action of the Board in shortlisting candidates who are not affiliated with any Department, the county flawed the recruitment process.

Mr. Speaker, the Committee findings were through the submission of the CPSB. The CPSB, Mr. Speaker, brought before the Committee files of all the recruits showing where they are currently working. This Report that shows the National Potato Council from Winnifred, Mukami Peter comes from Igembe South in Maua. He works with National Potato Council of Kenya. This information was generated from the file of this person, and so Mr. Speaker, the recruitment process was discriminatory because people were locked out especially those who saw the advert as internal and again did not apply because it was not external, Mr. Speaker.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The casuals of Kilifi, who have worked in this county for years, I want to remind our Leader of Majority who said that we have enough for lunch, breakfast and dinner, very true, Mr. Speaker. I will add that we are also in medical covers and house allowances. Let him know that the casuals we are trying to protect today are not enjoying medical covers and house allowances, Mr. Speaker. So, by them being recruited, Mr. Speaker, they will enjoy these amenities. Giving a room to someone who has not suffered the process of this harsh working conditions of this county, going months without salaries, Mr. Speaker, if he really cares, let him allow this process to be re-advertised so that we get those who have worked as casuals for years so that they can enjoy the dinner, lunch, breakfast, medical cover and house allowance that he is enjoying, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Mwambire): What about commuter allowances?

Hon. Ngirani: Everything, Mr. Speaker, you can add another one.

The Speaker (Hon. Mwambire): What about communication?

